JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA TARIME
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BOREGA

MKUU WA SHULE: 0766867646
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0768118555
S.L.P 186-TARIME-MARA

**KUMB: BRGHS/S.4969/2026/VOL/V-11** ………………

Ndugu; MZAZI/MLEZI WA ………………………………………..

S.L.P……………

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BOREGA………………

**A. UTANGULIZI**

1. Ninayo furaha kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi imemchagua binti yako Kujiunga na shule ya sekondariya wasichana **Borega** kwa kidato cha tano mwaka huu 2026 katika mchepuo wa HKL, HGLi, PCM, PCB na CBG.

2. **TAREHE YA KURIPOTI.**

Muhula wa masomo kwa wanafunzi wa kidato cha tano utaanza tarehe …………. Hivyo wanafunzi wote waliopangwa kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka…………… wanapaswa kuanza kuripoti shuleni kuanzia tarehe……………

. **Tafadhali jitahidi kufika shuleni tarehe iliyopangwa**

**3. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule hii ipo wilayani Tarime mkoani Mara Katika kijiji cha Borega kata ya ganyange karibu na mji mdogo wa Sirari ambao ni kilometa 17 mpaka shuleni.

Endapo utatumia barabara itokayo Mwanza kuja tarime utateremkia kituo kikuu cha mabasi cha Sirari, piah Wale wanaotokea **DAR ES SALAAM** wapande mabasi ya **BLUESTAR, NEW BESTLINE** na **ABOOD** na Wale wanaotoka Tanga, Manyara, Kilimanjaro na Arusha wapande mabasi ya **KIMOTCO**, na **LOLIONDO,** watatelemkia mji wa Tarime na watachukua gari ndogo kuelekea sirari (3,000) wakifika Sirari watachukua gari za kwenda Mugumu au Pikipiki (8,000) hadi shuleni.

kwa wale wanaotokea nje ya mkoa wa mara wanaofikia Mwanza wanapaswa kupanda magari katika kituo cha mabasi cha NYAMHONGORO yapo mabasi maarufu ya Zakaria, Bluestar, Smart luxury, na Kisire, ambayo hufika hadi sirari.

**4. KAULI MBIU**

Kauli mbiu ya Shule yetu ni **THE BEST GIFT IS KNOWLEDGE.** Hii ina maana kuwa zawadi nzuri ni Maarifa. Daima usiridhike na kiwango cha elimu ulichonacho, jaribu tabia ya kutamani kujifunza ili kuwa na maendeleo ya juu zaidi yatokanayo na juhudi, juhudi Katika masomo maarifa na nidhamu ili kuleta ufanisi na uwezo mkubwa wa kupambana na mazingira unayoishi.

Ili kufanikisha kauli mbiu hii kila mwanafunzi atatakiwa kujiheshimu, kuwaheshimu walezi/walimu na wanafunzi wenzake, kufanya kazi kwa bidi ndani na nje ya darasa, kujirekebisha Katika mwenendo, tabia na nidhamu.

Kwa heshima uliyopewa ya kuchaguliwa kujiunga na shule hii, unategemewa sana na shule, wenzako na jamii nzima ya hapa kuwa kielelezo kizuri cha shule yetu na Taifa kwa ujumla. Kanuni na sheria za shule zilizo ambatanishwa hapa zitakusaidia kufikia malengo yako. Kauli mbiu ya shule na madhumuni yako ya kuja hapa ni mwanga sahihi wa maisha yako ya baadaye.

**ZISOME KWA MAKINI SANA** na ufahamu kuwa kusoma ni kujifunza na kujifunza ni kufahamu, kufahamu ni kujituma na kujituma ni kazi na kazi ni uhai wako kwa jamii na Taifa.

1. **SARE ZA SHULE**
   - a) Sketi mbili (2) ndefu mpaka chini kwenye kifundo cha mguu idara ya maji sketi 1 na light blue (blue sista) 1 za rinda box, mchoro wa sketi utaambanishwa, kitambaa kizito kama hujaelewa wasiliana mkuu wa Shule
   - b) Mashati mawili 2 meupe mikono mirefu
   - c) Sweta 2 rangi ya kahawia 1 na blue 1 zenye nembo ya shule zinapatikana katika duka la shule kwa (15,000/=) kwa atakayehitaji
   - d) Viatu vya ngozi pea mbili visigino vifupi vya Kamba
   - e) Soksi nyeupe ndefu (stocking) pea mbili 2
   - f) Raba za michezo pea moja (1) rangi nyeupe
   - g) Sketi ya blue pea moja ya michezo pair 1 mshono wa solo kitambaa aina ya babi
   - h) Track suti rangi ya blue pea moja ikiwa na t-shirt yake ndani kwaajiri ya usiku na wakati mwingine yenye nembo ya shule na inapatikana katika duka la shule.
   - i) T- shirt pea mbili rangi ya njano 1 na nyekundu 1 yenye material ya tujenge yenyenembo ya shule zinapatikana katika duka la shule
   - j) kwa waislamu shona vijuba vyeupe 2 utavyovalia kwenye sare ya shule. Na vyeusi 2 utavyovalia kwenye gauni la kushindia (shamba dress)

k) Shamba dress mbili rangi ya damu ya mzee (Maroon) iliyokolea mshono wa solo ndefu mpaka chini (gauni lakuvaa wakati kazi za usafi na nje ya masomo) kitambaa aina ya babi

l) Kulingana na maeneno yetu ni ya baridi, mtoto atakuta mzula shuleni wenye nembo ya shule kwa gharama ya tsh 10,000/=. Pia aje na sweta za mtumba nzito zisizo na maandishi rangi ya kijivu 1 na rangi nyeusi 1

m) **NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI**.



Vitambaa hivi ni vya sketi

T-shirt

2.





T-SHIRT

3. MICHANGO MBALIMBALI

| Na | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

4. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KULETA SHULENI..

i. Ream paper 2 A4 (double A) kwa mwaka

ii. Vitabu vya masomo kwa Tahasusi husika (Combination). Mfano kwa shule hii ni CBG, PCB, PCM, HGLi na HKL hivyo mwanafunzi anunue vitabu kulingana na tahasusi aliyo pangiwa.

iii. Dissecting kit Kwa wanafunzi wa somo la Biologia.

iv. Scientific Calculator fx 991

v. Godoro 1 la futi tatu lenye unene wa nchi 4 linalofaa kwenye kitanda cha chuma

vi. Shuka pea moja ;- kipande kimoja light blue na kipande kimoja PINK na foronya zake.

vii. Blanketi moja, tauro moja, khanga pea moja ya kuogea na night dress na chandarua.

viii. vyombo vya chakula (Sahani isiyo ya bati, kijiko, kikombe, bakuli, ndala na toilet paper kwa ajili ya matumizi yake.

ix. Ndoo 2 ya lita 20 (1) na lita 10(1), beseni (dishi) la kuogea moja na kidumu cha lita tano kwa ajili ya kuwekea

maji ya kunywa kwaajili ya matumizi yake binafsi.

x. Pedi pakt 10

xi. File mbili la kutunzia kumbukumbu zake ofsini(Aina ya plastic file). la kutunzia

nyaraka zake mwenyewe (Box File)

xii. Vifaa vya usafi kwa tahasusi ya PCB na CBG kwanja 1, jembe na mpini wake 1, mfagio

(hard bloom ndefu) mmoja, dawa ya choo kwa ajili ya usafi (ARO)

xiii. Kwa tahasusi ya PCM HGLi na HKL squeezer 2 na fagio ndefu za kuti za nje 1 na hardbroom 2 (mfagio mgumu Mrefu) , reki moja na dawa ya mbu(rungu 750mls) moja

xiv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

xv. Aje na nakala ya result slip au Cheti cha form four

xvi. Aje na madaftari ya kutosha (Kaunta books) Msomi 5, kalamu za kutosha, rula moja na mathematical set.

Kiwi, dawa ya meno, mswaki na brush.

xvii. Picha (Passport) nne za ndugu na wazazi watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi shuleni.

xviii. Aje na taa ndogo ya Sola kwa matumizi binafsi itamsaidia pindi umeme utakapo katika hii ni LAZIMA

xix. Sanduku la chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake (Tranka) sio begi wala sanduku kubwa lenye thamani kubwa.

xx. kama ni mgonjwa aje na cheti cha daktari

xxi. Aje na pesa ya matumizi kwa ajili ya matumizi yake binafsi na akifika akabidhi kwa Mwalimu.

5. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

I. Wizi

II. Kutohudhuria masomo kwanzia muda wa siku 90 bila taarifa/utoro

III. Kugoma na kuhamasisha mgomo

IV. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla

V. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote

VI. kufuga ndevu, kufuga nywele, Kusuka.

VII. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa yakulevya.

VIII. Uvutaji wa sigara, bangi na madawa ya kulevya

IX. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

X. Kupata ujauzito au kutoa mimba.

XI. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

XII. Kusababisha au kumpa mimba msichana.

XIII. Kutembelea majumba ya starehe (nyumba ya kulala wageni).

XIV. Kumiliki, kukutwa, au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

XV. Kucjhezea,Kudharau, huharibu fedha,bendera ya Taifa au picha ya viongozi .

XVI. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

XVII. Uharibifu wa mali za umma kwa maksudi.

XVIII.Kukataa, kugomea adhabu uliyopewa na viongozi

NB

a) Mwanafunzi harusiwi kuja na nguo za nyumbani.

b) Mzazi na mlezi pamoja na mwanafunzi soma kwa makini sheria no XIV na uielewe vizuri kwani kunafaini ya TSH 50,000/= Itakayotolewa na mzazi kwa kosa hilo ili kamati ya nidhamu kuweza kujadili tatizo hilo kwenye bodi ya shule.

c) Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ama kusuka nywele.

6. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII KWA MWANAFUNZI**

I. Ni lazima kusimama na kumsalimia mwalimu, mfanyakazi au mtu yeyote anaye kuzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano

II. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kwa wanafunzi wenzake, kwa walimu wake na watu wengine akiwa ndani au nje ya shule.

III. Ni lazima waheshimu bendera ya nchi na serikali, picha za viongozi wa chama na serikali, nembo ya taifa, wimbo wa taifa na fedha yan taifa.

IV. Ni lazima kwa mwanafunzi kufanya majaribio yote.

V. Wanafunzi lazima waheshimu ukumbi wa mikutanoi mahali pa kulia chakula, ofsi za shule, mali binafsi na mali za umma.

VI. Ni lazima kwa m, wanafunzi kusimama, kunyosha mkono juu anapo uliza au kujibu swali.

VII. Wanafunzi ni lazima kukaaa kimya wakati wote wanpo kuwa darasani, wasitoke nje bila

ruhusa ya mwalimu au kiongozi alilyoko darasani.

VIII. Wanafunzi lazima wasafishe na kuyatunza mazingira ya shule.

IX. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuondoka shuleni bila kibali cha mwalimu, kujisadia ovyo, kutupa taka ovyo, kukatisha viwanja, kukata miti au maua.

X. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana au kwenda kwenye nyumba za watumishi bila kibali maalum kitachotolewa na mkuu wa shule tu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Jina la mkuu wa shule: TUNSUBILEGE LUKASA

HEADMISTRESS
BOREGA S.S
P.O. BOX 136 TARIME.

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**(To be completed by Government Medical Officer)**

To Medical Officer,

………………………………………

………………………………………

………………………………………

Ref……………………………………………………………………………… (Name of student)

Please examine the above named student as per Medical examination form below

Full Name: ___________________________Age ______ Height ______(cm) Weight ______(Kg)

1. Blood count………………………………………………………………………………
2. Stool Examination………………………………………………………………………
3. Urinary (Pregnancy)……………………………………………………………………
4. STDs and Leprosy test…………………………………………………………………..
5. T.B and Leprosy test……………………………………………………………………
6. Eye Test…………………………………………………………………………………
7. Ear Test……………………………………………………………………………………
8. Chest………………………………………………………………………………………
9. Abdomen…………………………………………………………………………………
10. Spleen……………………………………………………………………………………

Any addition information: E.g. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g. Sickle cell), in ability to eat certain foods etc.

………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

I have examined the above named student and I certify that he/she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

………………………………...                                        ……………………….

Signature and Official Stamp                                        Date

Station…………………………..                                        Designation……………………….

**NB: FOMU HII IREJESHWE SHULENI WAKATI WA KURIPOTI**

# OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI
# HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI

11. JINA LA UKOO _________________ JINA LA KWANZA ____________ JINA LA KATI ____________
12. JINA LA MZAZI/MLEZI ________________________________ NAMBA YA SIMU ________________
13. KAMA NI MLEZI: UHUSIANO ____________________________________________________________
14. ANUANI YA KUDUMU YA MZAZI/MLEZI _____________________
15. TAREHE YA KUZALIWA __________________________
16. MAHALI MWANAFUNZI ALIPOZALIWA: KIJIJI CHA _________________ KATA YA ____________
    WILAYA __________________ MKOA WA ____________________
17. DINI ____________________ DHEHEBU ___________________
18. UNAINGIA KIDATO CHA ____________ TAREHE/MWAKA ___________________
19. KUTOKA SHULE YA MSINGI/SEKONDARI ______________________ WILAYA _______________
    MKOA _________________
20. MZAZI/MLEZI WAKO ANAFANYA KAZI YA AJIRA/MKULIMA/BIASHARA.
21. NDUGU WENGINE AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA HABARI MUHIMU JUU YAKO.
    i. _________________________ UHUSIANO ____________ NAMBA ZA SIMU _________
    ii. ________________________ UHUSIANO ____________ NAMBA ZA SIMU __________
    iii. ________________________ UHUSIANO ____________ NAMBA ZA SIMU _________
22. SIFA MAALUM KAMA UNAZO __________________________________________________________
23. TAARIFA ZA WAZAZI: (Weka alama ya Vema panapohusika)
    i. WAPO WOTE
    ii. YUKO MMOJA (TAJA - BABA/MAMA)
    iii. WOTE WAMEFARIKI

Nakiri kuwa maelezo yayolipo hapo juu ni sahihi.

SAINI YA MWANAFUNZI ………………__SAINI YA MZAZI/MLEZI ……………….

**AHADI YA MWANAFUNZI**

MIMI (Jina la mwanafunzi) ______________________ nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga katika shule hii. Naahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote zilivyotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

MIMI (Jina) ______________________________ ambaye ni mzazi/mlezi wa Mwanafunzi ________________ nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari wasichana Borega ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa Shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia mwema wa Taifa letu.

**NB: FOMU HII IREJESHWE SHULENI WAKATI WA KURIPOTI**

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BOREGA

### KIAPO CHA MWANAFUNZI.

Mimi (Jina La Mwanafunzi)……………………………………………Nakubali Kwa Dhati Kabisa Nafasi Niliyopewa Na Taifa Kujiunga Na kidato cha tano katika Shule ya sekondari Borega ilioko wilayani Tarime Mkoa wa Mara. Naahidi Kufuata Sheria Zote Za Shule Na Taratibu Zote Kama Zilivyotolewa Na Zitakavyotolewa Na Uongozi Wa Shule Ya Sekondari Borega.

Saini Ya Mwanafunzi……………………………… Tarehe…………………………………

### KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi)........................................................................ Ambaye Ni Mzazi/Mlezi Wa Mwanafunzi………….…………………………………….Nimeyasoma Masharti Na Sheria Zote Za Shule Ya Sekondari Borega ilioko wilayani Tarime Mkoa wa Mara Ambako Kijana Wangu Amechaguliwa Kujiunga na kidato cha tano.Naahidi Kwamba Nitamhimiza Mwanangu Kufuata Sheria Na Taratibu Zote Za Shule. Aidha Naahidi Kushirikiana Na Uongozi Wa Shule Katika Malezi Bora Ya Mwanangu Ili Baadaye Awe Raia Bora Na Mwema Wa Taifa Letu.Pia naahidi kumlipia ada na michango mingine ya shule.

Saini Ya Mzazi/Mlezi……………………………… Tarehe………………..

# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BOREGA

# ORODHA YA VITABU VYA KUNUNUA

Kila mwanafunzi anatakiwa kununua anghalau vitabu viwili kwa kila tahasusi

## HISTORY

1. Essentials in Advanced level History Paper 2 Based in new (2010) Syllabus, Written by Saleh Yasin
2. Contemporary History Events Volume 1. Writen by Shibitali CK. Tumain, Shibitali and Son Publisher.

## GEOGRAPHY

1. ZISSIT NEW SYLABUS
2. HARUNA MASENZA NEW SYLABUS ( LAZIMA)
3. MSABILA NEW SYLLABUS

## ENGLISH

1. Advanced Level English:A Practical A proach(Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper two)
2. Oxford Advanced Learner's Dictionary
3. NOVEL (ANIMAL FARM, AN OPPORTUNIST ELITE
4. PLAY ( AN ENEMY OF THE PEOPLE, THE HORIZON UNVEILED)
5. POETRY ( SUMMONS)

## KISWAHILI

1. Jikumbushe Kiswahili 2Kidato cha 5&6 Maswali na majibu by Eliupendo W.Mbise na Leonard Mbikilwa.
2. RIWAYA( DUNIA UWANJA WA FUJO, MIRATHI YA HATARI)
3. TAMTHILIYA ( USALITI MJINI, MKWAVA WA UHEHE)
4. USHAIRI ( MALENGA WA ZIWA KUU, WOSIA WA BABA)

## PHYSICS

1. TOM DUNCAN, S. CHAND'S For Class XI and XII,
2. ADVANCED LEVEL PHYSICS ( Principle of Physics) By M. Nelkon,
3. COMPREHENSIVE PHYSICS.
4. Review Physics One and Two. ZINGATIA MTAALA MPYA
5. Graph Pads –(FOUR)

4. Mathematical Set And Non Programmable Scientific Calculator kwa wanafunzi mchepuo (PGM)

## MATHEMATICS

1. Pure Mathematics1& 2 by Backhouse.J.K
2. Advanced Level pure mathematics (Fourth edition)by Tranter,CJ
3. S Chand's Mathematics Revised By Dass.H.K

***(Viambatanisho A,B,na C vijazwe na kurudishwa shuleni)***